**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako**


***Andika insha ya kusisimua juu ya:***

**NCHI YETU**

Compiled & Distributed by Schools Net Kenya P.O. BOX 15509-00503, Nairobi
Tel 0734579299 E-mail: infosnkenya@gmail.com ORDER ANSWERS ONLINE at
www.schoolsnetkenya.com

**Swali la 1 hadi la 5**

**Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.**



| | | |
|---|---|---|
| **Lisa** | : | Sabalkheri Baraka? |
| **Baraka** | : | Aheri Lisa. Habari za muda sahibu? |
| **Lisa** | : | Njema. ***(Akiyaangalia mavazi yake)***. Unaelekea wapi? |
| **Baraka** | : | Ninaelekea kwenye mazoezi ya mchezo wa kandanda. |
| **Lisa** | : | Hakika unapenda soka. |
| **Baraka** | : | Ndiyo. Mpira wa miguu unaimarisha viungo vya mwili, ubunifu na ushirikiano. Isitoshe, unaburudisha. Unaweza pia kukupa kipato maishani. |
| **Lisa** | : | Kipato? Kumbe mchezo wa kubumbu una manufaa mengi hivi? |
| **Baraka** | : | Ndiyo, Lisa. Si hayo tu. Mchezo wa gozi pia hukuza uwezo wa kufikiria kwa kina na kutatua matatizo hasa unapokabiliwa na wapinzani wako wakati unataka kuwashinda. |
| **Lisa** | : | Aha! Sasa nimefunguka macho zaidi. Asante kwa kunielimisha. |
| **Baraka** | : | Hewalla! Nawe unapenda mchezo upi? |
| **Lisa** | : | Ninapenda mchezo wa sataranji. |
| **Baraka** | : | ***(Kwa mshangao)*** Sataranji? Nilifikiri ungetaja mpira wa pete, mpira wa kikapu au hoki ! |
| **Lisa** | : | ***(Akitabasamu)*** Ni mchezo mzuri. Unajua kuwa mchezo huu pia hunoa akili? |
| **Baraka** | : | Aha! Sikuyafahamu hayo. Asante Lisa. |
| **Lisa** | : | Hewala! Sote tumeelimishana. Hakika elimu ni bahari! |
| **Baraka** | : | Kweli mwandani wangu. Kwaheri! |
| **Lisa** | : | Kwaheri ya kuonana. ***(Wote wanaondoka)***. |

1. Badala ya sabalkheri, Lisa pia angesema, ______________________________?

   A. hujambo B. umeamkaje

   C. shikamoo D. salama

2. Ni neno lipi la adabu alilotumia Lisa katika mazungumzo haya?

   A. Kumbe B. Hakika

   C. Asante D. Aha!

3. Sentensi zifuatazo zimetumiwa katika mazungumzo haya. Ni sentensi ipi inayoonyesha kuwa Baraka anakubaliana na alichosema Lisa?

A. Ninaelekea kwenye mazoezi ya mchezo wa kandanda.

B. Unaweza pia kukupa kipato maishani.

C. Mchezo wa gozi pia hukuza uwezo wa kufikiria kwa kina.

D. Kweli mwandani wangu. Kwaheri.

4. Je, ungeyasikiliza mazungumzo ya Baraka na Lisa, ungejifunza nini?

A. Ni sharti ushiriki katika mchezo wa kabumbu ili utambulike.

B. Ni muhimu kubadilishana mawazo kuhusu mambo tunayoyajua.

C. Kufikiria kuhusu michezo kunapunguza matatizo.

D. Kufahamu aina zote za michezo kunamletea mtu fahari.

5. Katika mazungumzo haya mchezo wa kandanda umepewa majina mbalimbali. Majina kama haya huitwaje?

A. Vitate | B. Vitanzandimi

C. Visawe | D. Silabi

**Swali la 6 hadi la 8**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**



Ukosefu wa mvua umesababisha madhara yasiyomithilika . Ukame unapojiri wanyama na mimea ndiyo inayoathiriwa zaidi na joto. La muhimu kujiuliza ni je, ikiwa wanyama wanaathirika hivyo sembuse binadamu? Mojawapo ya viini vya hali hii ni hulka ya binadamu ya kutozingatia suala la kuongeza thamani katika mazingira kwa kuyatunza. Matokeo ya hulka hii ni kwamba watu wengi wameshindwa kujitosheleza hata kwa mahitaji ya kimsingi kama vile chakula. Wengine wanakuwa maskini ombaomba kwa kuuza ardhi yao kiholela.

6. Ni jibu lipi sahihi kulingana na aya ya kwanza?

A. Ukosefu wa mvua hauleti madhara mengi.

B. Wanyama na mimea huathiriwa zaidi na ukame.

C. Wanyama huathiriwa na ukame zaidi kuliko mimea.

D. Wakati wa ukame hakuna joto jingi.

7. Gani kati ya haya si matokeo ya ukosefu wa mvua?

A. Mimea kukauka | B. Ukosefu wa maji

C. Kufa kwa wanyama | D. Watu kuwa matajiri

8. Neno lenye maana sawa na hulka ni ____________________

A. tabia | B. heshima

C. nidhamu | D. bidii

**Swali la 9 hadi la 12**

***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

Alivyoniumba Mungu, kamwe mimi sikatai,
Wakubali moyo wangu, kuupinga hakufai,
Ajua jinsia yangu, mjenzi wangu msingi,
Nimetosheka nilivyo, najionea fahari.

Ona fanaka zangu, nimefua dafu kwingi,
Kutoka mtima wangu, nimewafadhili wengi,
Na hii jinsia yangu, asilani haipingi,
Nimetosheka nilivyo, najionea fahari.

Jiamini ndugu yangu, aidha waweza mengi,
Na katika ulimwengu, wataka hekima nyingi,
Ibuka ewe mwenzangu, wasiwasi haujengi,
Nimetosheka nilivyo, najionea fahari.

9. Shairi hili linazungumzia suala gani?
   A. Jinsia
   B. Ubaguzi
   C. Uwajibikaji
   D. Heshima


10. Kwa mujibu wa shairi hili, si kweli kusema kuwa
    A. kila mshororo katika ubeti wa kwanza una mizani kumi na sita.
    B. vina vya kati vya ubeti wa pili ni, "ngu, ngu, ngu, vyo."
    C. shairi hili lina beti tatu.
    D. mshororo wa mwisho katika kila ubeti haufanani

11. Nini maana ya , 'najionea fahari,' kulingana na kifungu hiki?
    A. Najivunia
    B. Naona haya
    C. Nina wasiwasi
    D. Ninahuzunika

12. Katika ubeti wa tatu mshairi anamhimiza msomaji kufanya nini?
    A. Kujiona bora
    B. Kujidharau
    C. Kuogopa
    D. Kufaulu

**Swali la 13 hadi la 15**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**



Herini, mkufu, kipini, kidani na pete ni aina za mapambo. Mapambo haya huvaliwa sehemu mbalimbali za mwili. Kazi yake ni kumfanya mtu wa jinsia yoyote avutie zaidi.

Herini huvaliwa masikioni hasa na wanawake. Mkufu huvaliwa shingoni. Pambo hili linaweza kuvaliwa na jinsia zote. Kidani huvaliwa pamoja na mkufu. Kwenye upande wa pua, wanawake huvaa kipini. Hatimaye pete huvaliwa kidoleni na wanawake pamoja na wanaume.

Darasani wanafunzi wanaposoma kuhusu mapambo pia hujifunza fani za lugha. Katika vitendawili pambo mkufu hutumika kujibia kitendawili, 'dhahabu yangu ya thamani haisimami.' Pambo pete hutumika katika tashbihi isemayo, 'pendana kama chanda na pete.'

**13.** Kulingana na aya ya kwanza, kazi ya mapambo ni gani?

A. Kuvaliwa na jinsia yoyote

B. Kuongeza urembo

C. Kuvaliwa kama nguo

D. Kutofautisha jinsia

**14.** Ni mapambo gani huvaliwa na jinsia zote?

A. Herini na kipini

B. Mkufu na kipini

C. Mkufu na kidani

D. Kipini na kidani

**15.** Kulingana na kifungu

A. majina ya mapambo huchangia katika kujifunza fani za lugha.

B. mkufu si mojawapo ya majibu ya vitendawili.

C. pendana kama chanda na pete ni aina ya pambo.

D. chanda ni pambo linalovaliwa kwenye pete.

**Swali la 16 hadi la 20**

**Soma kifungu kifuatacho. Kwa kila swali umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Ujenzi __16__ taifa unahitaji ushirikiano wa wananchi __17__. Wahenga walisema kuwa umoja ni __18__. Kila mwananchi __19__ kazi asiwe mvivu au __20__.


| | | | |
|---|---|---|---|
| **16. A.** ya | **B.** wa | **C.** la | **D.** cha |
| **17. A.** sote | **B.** lote | **C.** wote | **D.** zote |
| **18. A.** ngao | **B.** udhaifu | **C.** upendo | **D.** nguvu |
| **19. A.** anapochapa | **B.** anapopiga | **C.** anapokula | **D.** anapolaza |
| **20. A.** mvuvi | **B.** mzembe | **C.** mpole | **D.** mkali |


**Swali la 21 hadi la 30**

**Chagua jibu sahihi.**

**21.** Hizi ni picha za michezo mbalimbali. Ni upi haujaambatanishwa na jina lake sawasawa?

A.  Chesi

B.  Jugwe

C.  Soka

D.  Kandanda

22. Hili ni jedwali la maneno. Chagua jibu linaloonyesha viwakilishi vya nafsi?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| A. | ambaye | ambacho | ambalo | ambao |
| B. | cheza | lima | andika | pata |
| C. | moja | chache | nyingi | kumi |
| D. | wewe | sisi | nyinyi | wao |

23. Maneno haya yanafuatana vipi katika kamusi?

***i) karatasi***

***ii) karakana***

***iii) karani***

***iv) karamu***

A. (iv), (i), (iii), (ii)

B. (ii), (iv), (iii), (i)

C. (iv), (iii), (ii), (I)

D. (ii), (i), (iv), (iii)

24. Ni jina lipi lililo katika ngeli tofauti?

A. Maji

B. Magari

C. Mafuta

D. Maziwa

25. ***<u>Chagua jibu ambalo ni wingi wa sentensi:</u>***

Ua wa nyumba yangu una ua zuri.

A. Nyua zä nyumba zetu zina maua mazuri.

B. Maua ya nyumba yangu yana maua mazuri.

C. Nyua za nyumba zetu zina maua nzuri.

D. Ua wa nyumba zetu una maua mazuri.

26. Chagua jibu ambalo lina maneno ambayo ni visawe.

A. Mgeni - Mwenyeji

B. Ndege - Nyuni

C. Rafiki - Adui

D. Ajuza - Shaibu

Compiled & Distributed by Schools Net Kenya P.O. BOX 15509-00503, Nairobi
Tel 0734579299 E-mail: infosnkenya@gmail.com ORDER ANSWERS ONLINE at
www.schoolsnetkenya.com

27. Chagua jibu linalounganisha sentensi hizi kwa usahihi.

***i) Juma alimpikia Zawadi sima.***

***ii) Zawadi alimpikia Juma sima.***

A. Zawadi alipikiwa sima kwa Juma.

B. Zawadi alipikia sima kwa Juma.

C. Zawadi na Juma walipikiana sima.

D. Juma na Zawadi walipikiwa sima.

28. Chagua sentensi ambayo ni ukanusho wa: Wakulima watapanda mahindi shambani.

A. Wakulima hawakupanda mahindi shambani.

B. Wakulima hawangepanda mahindi shambani .

C. Wakulima hawajapanda mahindi shambani.

D. Wakulima hawatapanda mahindi shambani.

29. Ni sentensi ipi iliyo katika hali ya udogo?

A. Kijiji hicho kina watu wengi.

B. Kiatu cha babu yake kimepotea.

C. Kibeti kimenunuliwa na mama.

D. Kisu cha mama kinavutia.

30. Chagua jibu lenye maana sahihi ya nahau.

| | | |
|---|---|---|
| A. Kula kikoa | - | Shirikiana kufanya kazi. |
| B. Changa bia | - | Fanya biashara. |
| C. Piga jeki | - | Gawa sawa. |
| D. Fanya bidii | - | Acha kufanya kazi. |

Compiled & Distributed by Schools Net Kenya P.O. BOX 15509-00503, Nairobi
Tel 0734579299 E-mail: infosnkenya@gmail.com ORDER ANSWERS ONLINE at
www.schoolsnetkenya.com